na Michael Matemanga

MWANANCHI UK 4

# Ngozi za ng'ombe, nguruwe kutumika matibabu ya moyo

Baraka Loshilaa, Mwananchi
bloshilaa@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Kwa mara ya kwanza wagonjwa wenye tatizo la kuziba kwa mshipa mkubwa wa damu ndani ya moyo wameanza kutibiwa kwa njia ya tundu dogo katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI)

Kupitia teknolojia hiyo mpya ambayo kifaa maalumu huingizwa hadi kwenye mshipa husika na kuweka valvu inayotengenezwa kwa ngozi ya ng'ombe au nguruwe, tayari wagonjwa watatu wamekwishatibiwa.

Awali, wagonjwa waliobainika kuwa na maradhi hayo ya moyo, walifanyiwa upasuaji wa kufungua kifua na kubadilisha valvu ya mshipa mkubwa wa damu, sasa huduma hiyo itaendelea kutolewa lakini itawahusu vijana pekee.

Akielezea teknolojia hiyo, Daktari bingwa wa matibabu kwa njia ya tundu dogo JKCI, Khuzeima Khunbhui alisema huduma hiyo itawanufaisha watu wenye umri wa kuanzia miaka 70 na kuendelea.

"Kipindi cha nyuma tulifanya upasuaji kufungua kifua na kuweka valvu kwenye mshipa wa moyo (kwa wagonjwa wote, wakiwemo wa miaka 70 na kuendelea), lakini sasa tutatumia njia ya tundu dogo kuweka valvu hiyo kwenye mshipa wa moyo ulioziba.

"Valvu hii inayotengenezwa kwa kutumia ngozi ya ng'ombe au nguruwe, ina uwezo wa kudumu kwa miaka 15 kwenye mshipa wa moyo," alisema daktari bingwa huyo.

Alisema utafiti unaendelea duniani kuangalia kama valvu zinazowekwa sasa zinaweza kudumu zaidi ya miaka 15, endapo vijana watawekewa.

Alifafanua kuwa, tiba wanayopata vijana wenye matatizo hayo ni kuwekewa chuma ndani ya mshipa wa moyo, ambacho kinadumu kwa muda mrefu huku mgonjwa akitakiwa kutumia dawa kwa maisha yake yote.

Alisema kama vijana watatibiwa kwa njia ya tundu dogo, itawahitaji kufanyiwa mabadiliko ya valvu watakayowekewa kila baada ya miaka 15.

**TIBA >**

## Jinsi upasuaji huo unavyofanyika

**Upasuaji wa mshipa mkubwa wa moyo kwa njia ya tundu dogo, ni kumfanyia mgonjwa upasuaji mdogo wa moyo wa kubadilisha valvu ya mshipa mkubwa wa damu yenye tatizo.**

**Njia hiyo haihusishi kufanya upasuaji wa kufungua kifua, bali mgonjwa hufika wodini siku ya kwanza na kufanyiwa matibabu hayo kwa kutoboa tundu kifuani au mguuni karibu na goti.**

**Valvu hiyo huingizwa hadi kwenye mshipa mkuu wa moyo wenye tatizo baada ya kuuzibua.**

### Ushuhuda mgonjwa

Donald Lema wa Machame, Kilimanjaro akisimulia namna alivyobaini ugonjwa huo, alisema kujisikia mwili kukosa nguvu na akitembea mita 100 lazima apumzike, hivyo alikwenda kufanya uchunguzi Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini, KCMC na kuambiwa valvu moja ya moyo ililegea,

"Niliambiwa matibabu ni India au JKCI, nilikuja JKCI na nimepatiwa matibabu na sasa naendelea vizuri, sikusikia maumivu eneo lolote la mwili," alisema.

Alisema gharama ya matibabu alipaswa kulipa Sh80 milioni lakini alilipa Sh25 milioni, kiasi kingine kiligharamiwa na Serikali.

### Kiini cha tatizo

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Moyo JKCI, Tatizo Waane alisema ugonjwa huo hutokana mabadiliko ya mwili.

Alielezakwa watu wazima tatizo hilo huchangiwa na umri mkubwa ambapo valvu husababisha kuzalishwa kwa madini chokaa ndani ya mshipa wa moyo.

"Chokaa hizo hujikusanya na baadaye hufanya damu kushindwa kutoka na kuingia kwenye moyo, hivyo figo, ubongo na viungo vingine mwilini huanza kupata damu kidogo na hivyo mhusika huanza kupata maumivu ya kichwa na kifua," alisema.

Dk Waane alisema kupitia njia ya tundu dogo, daktari humhudumia mgonjwa ndani ya saa moja hadi mbili na mgonjwa kuondoka wodini siku inayofuata, tofauti na upasuaji ambao mgonjwa hutumia zaidi ya wiki wodini.

Kuhusu gharama ya matibabu alisema, mgonjwa mmoja hapa nchini sasa atatibiwa kwa Sh80 milioni tofauti na nje ya nchi ambapo mgonjwa anatibiwa kwa Sh150 milioni.

### Uwezo wa watalaamu JKCI

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk Peter Kisenge alisema uwezo wa wataalamu ndani ya taasisi hiyo uliwezeshwa na wenzao wa Hospitali ya Starcare ya India.

Alisema madaktari wa JKCI kwa asilimia 90 wana uwezo wa kutoa huduma hiyo.

Alisema JKCI imeendelea kuwa kituo cha utalii tiba na wagonjwa kutoka nchi 20 za Afrika zinazofika kwenye taasisi hiyo kupokea matibabu.

Kutokana na wigi wa wagonjwa, Dk Kisenge aliiomba Serikali iipatie jengo lingine kwa ajili ya kuwahamishia wagonjwa, ombi ambalo Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk John Jingu alisema linafanyiwa kazi.

Dk Jingu alisema uwekezaji kwenye sekta ya afya una umuhimu mkubwa, akifafanua kuwa kwa mwaka huu Serikali imeweka Sh7 trilioni kwenye sekta ya afya.

Kwa upande wa wataalamu, alisema zaidi ya Sh10.9 bilioni zimewekezwa na Serikali kusomesha wataalamu kwenye nchi mbalimbali, ambao watakuja kutoa matibabu ya kibingwa nchini.

Kati Julai na Desemba mwaka huu, alisema JKCI imehudumia zaidi ya wagonjwa 3,000 na kuingiza Sh920 bilioni.

**Sh80 mil**
Gharama za upasuaji wa moyo kwa njia ya matundu madogo.

**Sh920 bil**
Kiasi cha fedha ambacho JKCI imeingiza kati ya Julai na Desemba 2023.

**3,000**
Idadi ya wagonjwa waliohudumiwa na JKCI kati ya Julai na Desemba 2023.

CamScanner



UFUGAJI

MWANANCHI UK 6

# Wafugaji waondolewa kero ya malisho

Bakari Kiango, Mwananchi
bkiango@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega amesema wafugaji hawana haja ya kuangaika kutafuta mbegu za malisho ya mifugo kwa sababu zipo za kutosha, baada ya Serikali kuzizalisha katika shamba lake la Kibaha mkoani Pwani.

Waziri Ulega amesema upatikanaji wa uhakika wa mbegu ikiwemo za Juncao zinazozalisha malisho yenye virutubisho na vitamini kwa ajili ya mifugo zitapunguza changamoto ya tabia ya baadhi ya wafugaji kupeleka mifugo katika mashamba na kusababisha mgogoro.

Waziri Ulega alitoa kauli hiyo juzi wakati wa ziara ya kutembelea shamba la mbegu na malisho ya mifugo la wizara hiyo lilipo Vikuge wilayani Kibaha. Katika ziara hiyo, Ulega aliambatana na timu ya wataalamu wa mifugo na malisho wa wizara.

Katika ziara hiyo, Waziri Ulega pia alitembelea kiwanda cha kuchakata mazao ya mifugo ikiwemo ng'ombe, mbuzi na kondoo cha Tan-choice na taasisi ya chanjo ya mifugo.

"Kama wafugaji waliokuwa wanahoji ni wapi watapata mbegu bora, jibu limepatikana sasa zipo hapa Vikuge na maeneo mengine tutakayotoa maelekezo," alisema.

Alisema mbegu hizo zenye mfano wa vipingili vya miwa zitakuwa zikiuzwa Sh4,000 kwa kilo, lakini siku zijazo Serikali itaangalia uwezekano wa kushusha bei ya mbegu, ili kuwezesha wafugaji wengi kuzinunua.

Kwa mujibu wa Ulega, hivi sasa kuna tani 78 za mbegu za majani aina ya Juncao, hivyo kuwataka wafugaji kuchangamkia fursa hiyo kwa kuzinunua na kuzipanda, ili kuwa na uhakika wa malisho katika misimu yote ikiwemo ya kiangazi.

"Tupande mbegu hizi ili tupunguze changamoto ya mifugo kufa au kukosa malisho au suala la mifugo kuvamia mashamba ya wakulima.Ni aibu kuendelea kuona wakulima wafugaji wanagombana tutafute suluhu ya malisho ya uhakika," alisema.

Kwenye ziara hiyo baadhi ya vikundi vya wafugaji kikiwemo cha Esther Moreto Renatha kilinunua mbegu za Juncao kilo 200 kwa ajili ya kupanda, ili kupata malisho ya uhakika ya mifugo.

Meneja wa shamba hilo, Ruben Ngailo alisema mbali na mbegu za Juncao, pia wamepanda nyasi lishe na kuna mtama lishe.

CS CamScanner